

336/2

KISWAHILI
Karatasi ya Pili
2024
Saa 2



UGANDA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

Uganda Certificate of Education

KISWAHILI

Karatasi ya Pili

Ufahamu na Uchambuzi wa Fasihi

Saa Mbili

MAAGIZO KWA WATAHINIWA:

Karatasi sehemu mbili; A na B.

Maswali yote ni ya lazima.

Majibu yote yaandikwe kwenye karatsi uliyopewa.

SEHEMU A

UFAHAMU

- Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.*

MGOMO SHULENI

Siku moja nilikutana na kijana aitwaye Odeke Musa katika kijiji cha Ryeru. Kijiji hiki kinajulikana sana kwa kuzalisha mahindi yanayotegemewa kwa mlo wa ugali unaotumiwa na takribani nusu ya raia wa nchi hii. Watu wengine hutambua kijiji hiki kama “jiko la taifa”. Kijana Odeke Musa kwa umri wake mdogo, anastahili kuwa shuleni akishughulikia masomo lakini mambo sivyo yalivyo.

Nililazimika kumwendea moja kwa moja na kuzungumza naye ili angalau nijue kisa na sababu ya kutokuwa shuleni. Uso wake, waziwazi ulikuwa ukionesha huzuni na masikitiko ya hali ngumu anayopitia. Tulipoanza kuzungumza machache hivi, machozi yalianza kumtiririka tiriri! Baada ya kupoa akanihadithia kwamba anajutia siku ile aliposhiriki na kuongoza mgomo shuleni pamoja na rafiki zake.

Kwa kawaida, mzaha mzaha hutumbua usaha. Mambo yenewe yalianza kimchezomchezo. Wanafunzi walianza kulalamikia hali mbaya wanayopitia hapo shuleni. Kwanza kabisa, walilalamikia chakula kibaya walichokuwa wakitayarishiwa, uhaba wa maji uliwalazimisha kutembea mwendo mrefu hadi kisimani nje ya shule kuchota maji. Pia walilalamikia ukosefu wa walimu wa kutosha. Pamoja na adhabu kali sana wanazopewa na walimu wao baada ya makosa madogo madogo.

Siku moja, majira ya saa saba usiku, wanafunzi walianzisha mgomo na kuharibu madarasa, nyumba za walimu pamoja na magari ya shule na mali nyingine nyingi. Kesho yake, uchunguzi wa kina ulifanyika. Iligunduliwa kuwa wanafunzi aliyejulikana kwa jina la Odeke Musa alikuwa miongoni mwa wanafunzi walioongoza mgomo. Bila shaka, sheria za shule hazikuwaruhusu wanafunzi wa tabia kama hizo shuleni. Odeke Musa alijikuta ametupwa nje ya lango la shule.

Wazazi wake walipopata habari kuhusu vitendo vya mtoto wao, walipandwa na hasira juu ya utovu wa nidhamu. Wazazi wake hawakujisumbua hata kumtafutia shule nyingine ili aweze kuendelea na masomo. Odeke Musa alianza kutafuta vibarua mbalimbali ili aweze kusukuma maisha yake. Alianza kufanya kazi za sulubu alizobahatika kupewa na yejote aliyemhurumia. Odeke Musa alionesha huzuni na majuto chungu nzima akasahau yaliyosemwa na wahenga kwamba ‘majuto ni mjukuu, huja baadaye’.

Kwa hakika, Odeke Musa alikuwa tayari kumwomba msamaha yejote yule aliyemkosea hasa viongozi wa shule na wazazi wake. Alijutia sana masomo yake na yale malengo aliyokuwa nayo kuitia elimu. Je, ni nani aliyekuwa tayari kumsamehe?

Miaka ilivyozidi kusonga, ndivyo matumaini yake ya kurudi shuleniyalivyozidi kuzama jii na kuzikwa katika kaburi la sahau. Maskini Odeke, alijifunza maana ya ‘mpiga ngumi ukuta humiza mkonowe’.

Hatimaye, alianza kufungua ukurasa mpya wa maisha. Akaanza kupanga na kushughulikia maisha bila elimu. Majengo ya shule aliishia kuyaona kwa umbali pamoja na kuwatamani wenzake waliokuwa wakivalia sare za shule. Kazi zake kubwa sasa ni za vibarua kama vile kulisha ng’ombe wa majirani zake, kufyeka nyasi kwa nyua, kuchimba vyoo, kuchotea watu maji na kazi nyinginezo za aina hiyo hiyo ili achume shilingi za kumfutia machozi.

Maswali:

- (a) Kulingana na taarifa hii, kwa nini Odeke Musa anajuta?
- (b) Ni hali gani ambazo zinaweza kusababishia wanafunzi kufanya fujo shuleniyalivingana na taarifa?
- (ch) Ni changamoto gani zinazoweza kumkumba mwanafunzi anayeshindwa kumaliza masomo yake?
- (d) Ni nini maoni yako kuhusu adhabu aliyopewa Odeke Musa baada ya mgomo shuleniyalivingana?

SEHEMU B
UCHAMBUZI WA FASIHI

- 4.** *Soma dondo hili kisha ujibu maswali yatakayofuata.*

(Ndani ya famasi ya Daktari Jackob. Amepanga dawa katika rafu za vioo na anapekua pekua kitabu cha wateja ambao anadai pesa.)

Selina: *(Akikimbia kuelekea famasi huku jasho Linamtoka. Ameva sketi ndefu yenye maua) Shikamoo! Daktari?*

Daktari Jackob: *(akishusha miwani yake) Marahaba! Mbona unatokwa jasho! Unakotoka ni kwema?*

Selina: *(Ameweuka mikono yake miwili juu ya kichwa.) La! kabisa! Mama yangu ni mgonjwa yuko katika hali mbaya.*

Daktari Jackob: Ameugua ugonjwa gani tena?

Selina: Ni ugonjwa wake uleule wa pumu ambao unamshika vibaya hasahasa wakati wa baridi nyingi kama leo.

Daktari Jackob: (*Akitandaza mikono*) Kwa hiyo nifanye nini?
Kwanza, ninashukuru Mungu kuwa umejileta hapa.
Isingekuwa hali mbaya ya mama yako, hungekuja. Kabla
hatujaenda mbali, unajua pesa ngapi unazodaiwa kwenye
kitabu hiki?

Selina: (*Kwa upole*)
Naam, ninajua lakini tafadhali Daktari, nimeacha mama
katika hali mahututi na hakuna mtu mwingine nyumbani.
Ninaomba unipe dawa, mengine tutayashughulikia baada
ya mgonjwa kupata nafuu.

Daktari Jackob: (*Kwa kejeli akimuonesha vidole vyote*)
Hebu sikiliza! Mama yako kupona na kufariki
hayanihusu. Ninachotaka hapa ni pesa zangu.
(*akipigapiga kidole kwa meza ya glasi*) ama sivyo,
hakuna dawa!

Selina: (*Akimwangalia kwa macho yake mazuri huku machozi yakimtiririka*) Daktari, nyumbani niko mtoto mmoja
pekee, sina baba wala jamaa ambaye anaweza kunisaidia.
Please nipe dawa mama yangu akipona nitaiza kuku
wangu wawili ili nianze kulipa pesa zako polepole.

Daktari Jackob: (*Huku akiwa ameweke kalamu mdomoni, akiangalia kifua cha Selina. Anamkodolea macho kimya kimya na kutabasamu kidogo*)
Naweza kukusaidia, ila kwa sharti moja tu! (*akionesha kidole kimoja*)

Selina: (*Akifuta machozi kwa matumaini*) Nitafuata sharti lolote
ikiwa litamsaidia mama yangu kupona. Niambie basi.

Daktari Jackob: (*akikitikisa kichwa*)
Good girl! Wewe ni msichana mrembo, mwenye sura
nzuri. Ukitumia mwili wako huwezi kukosa kitu!
Ninamaanisha, ukiniruhusu kuona umbo lako hili
(*akimsogelea na kugusa kifua chake*) nitakupa famasi
nzima.

Selina: (*Kwa ukali na uchungu, anamsukuma nyuma kwa nguvu karibu aanguke kwenye sakafu*) Siwezi kuuza mwili
wangu kwa ajili ya kupata dawa! Mungu aliyeniumba,
atanipa njia nyingine za kupata dawa ya mama yangu.
(*anaanza kutembea polepole kama mtu aliyefiwa*)

Maswali:

- (a) Fafanua mandhari ya onyesho hili.
- (b) Wasichana wa siku hizi wanapata maadili gani kutokana na sifa za Selina?
- (ch) Fafanua hisia unazopata baada ya kusoma dondoo hili?
- (d) Ungekuwa Selina, ungetumia njia gani bora ya kupata dawa ya kumtibu mama yako?
- (e) Chambua mbinu za uandishi ambazo zimetumiwa na mwandishi wa dondoo hili.